

Je,  
**Nidhamu  
inayojenga**  
ni ipi?



Jishindie kompyuta  
ndani!







Viboko  
havisaidii  
kubadili tabia  
ya watoto.  
Huwafanya  
wawe waoga  
na washindwe  
kutambua  
mazuri na  
mabaya. Ni  
kutumia  
mamlaka  
vibaya...

Wewe, hebu  
kafanye kazi  
zako!

Sawa  
mwalimu!



Fagia hili  
darasa!

Sawa  
mwalimu!

Viboko  
humlazimisha  
mtoto  
akuheshimu  
kwa uoga,  
lakini  
havimsaidii  
kujitambua  
na kujua  
zuri na baya.

Wanafunzi watatumiq muda mwingi  
kuwaza namna ya kukwepa  
adhabu badala ya kubadili tabia

Niruhusu niangalizie  
jibu lako basi...

Hapana!



Lakini mwalimu yuko  
nje, hatajua nimeibia!


Viboko havisaidii kujenga uelewa  
wa wanafunzi kutambua lipi zuri au  
baya.

Iwapo tunataka kuwasaidia  
wanafunzi kujifunza kupitia  
makosa, tunapaswa kuwalea  
katika nidhamu isiyowajengea  
uoga!



## Nidhamu inayojenga hujumuisha:




- 
1. Kufikiri kabla ya kutenda
  2. Kufikiri na kuwa na malengo ya muda mrefu
  3. Kuwa na msimamo
  4. Kujiamini
  5. Uvumilivu
  6. Ubunifu
  7. Uaminifu.



Stadi hizo zinatusaidia kufanya maamuzi mazuri yanayotusaidia kufanikiwa katika maisha.



Wana lengo madhubuti,



...wanajiamini,



...wanafanya kazi kwa bidii,




...wanafikiri mbinu mpya za kutatua matatizo,



na wana msimamo.



Mtu mwenye Mambo yote haya kwa pamoja, husemekana kuwa mwenye nidhamu ya ukweli!



Nidhamu inayojenga hutoka ndani ya mtu,



Hutegemeana na jinsi tunavyo jihisi wenywewe.



Watu waliofanikiwa hujifunza mbinu hizi mapema kutoka kwa wazazi na walezi,

Lakini la muhimu zaidi, hujifunza mbinu hizi shuleni pia.



Ni sahihi!

Shuleni kwetu tunasisitiza nidhamu inayojenga madarasani!

2. Tunapinga vikali ukatili. Hatudhalilishi wala kuwatisha wanafunzi.



## Hulenga katika kurekebisha tabia,

Umfanya vizuri kuvalaa sare za shule leo...  
Lakini kesho, hakikisha ni safi pia!



## ...sio kuwadhalilisha wanafunzi

Unapenda kuwa mchafu, sio? Sasa,  
vaa na hili tambara siku nzima!



## ...hulenga katika kumsaidia mwanafunzi kujifunza,

Sasa andika insha  
kuhusu madhara ya  
udanganyifu.



## na sio kuwanyanyasa kwa makosa yao.

Mwongo wewe!  
Utakoma, viboko 50!





## Kusisitiza nidhamu inayojenga, hujumuisha hatua 4 za uwajibishaji tunaotumia

### Fidia ya makosa

Kuwawajibisha wanafunzi kwa makosa yaliyosababisha uharibifu.

### Tafakari

Huwasaidia wanafunzi kufikiri kuhusu tabia zao kutohana na makosa yao madogo madogo ya kila siku.

### Adhabu

Kuwaadhibu wanafunzi ili kutambua athari za makosa yao yanayojirudia mara kwa mara.


### Hatua ya Mwishi

Mpatie adhabu mwanafunzi kwa makosa makubwa ili kumrudi.

Hii pia ni moja ya mbinu ya kuwasaidia.

## Tafakari:

Ili kuwasaidia wanafunzi kuweza kutafakari kuhusu makosa yao madogomadogo ya kila siku, tumia mbinu zifuatazo...





## Adhabu:

Ili kumsaidia mwanafunzi kuelewa madhara ya kufanya makosa ya mara kwa mara, tumia mbinu zifuatazo...





**Uwajibishwaji:**  
Ili wanafunzi wajutie makosa yao  
yaliiyosababisha uharibifu, tumia mbinu  
zifuatazo...



37



38



### Hatua ya Mwisho:








Tunasimamia usahihi na kuweka sera nzuri.




Kuwajengea mazingira ambayo watoto wanaelewa undani wa maadili na mienendo wanayofundishwa kushika.  
Tunasisitiza nidhamu isiyo ya uoga katika utawala pia.


Viwango ni jumla ya mambo ambayo shule yetu huzingatia. Huelezea dira yetu ya kuwa na shule bora.



Wanatusaidia kuwa na tabia njema.



Tuliandika malengo...



na kuyabandika katika maeneo ya shule.



Tunayasema kwa pamoja mstarini!

Tunajivunia shule yetu nzuri!



Nidhamu sahihi katika utawala hujumuisha kutengenezwa kwa sheria na taratibu zitakazosaidia kufikia maaazimio yaliyowekwa.

MAAZIMIO	SHERIA
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tunajivunia shule yetu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Hakuna kutupa takataka ovyo</li> <li>- Hakuna kuharibuu mali za shule</li> </ul>
<ul style="list-style-type: none"> <li>• Tunaheshimu kila mtu</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>- Hakuna kunyanyasana</li> <li>- Hakuna kupigana</li> <li>- Hatukubali adhabu za bakora</li> </ul>

Sheria hizi huwekwa katika mwongozo unaoelezea majukumu na wajibu wetu,



## Vilevile mambo yanayopigwa marufuku...

- Hakuna utoro darasani
- Hakuna kuvuta sigara
- Hakuna kuibia mitihani

## Na kuhakikisha kuwa hatua za kinidhamu zinachukuliwa...

- ✓ Msamaha
- ✓ Kutolewa nje kwa muda
- ✓ Maonyo
- ✓ Kisanduku cha wakosefu
- ✓ Adhabu ya kazi
- ✓ Kuzuiliwa shulenii kwa muda
- ✓ Kuandika barua
- ✓ Kuita wazazi

Nidhamu ijengayo katika utawala vilevile humaanisha kuwa kila mtu anafahamu maazimio na sera,



na tunashirikiana  
pamoja  
kuyahimiza.



Watoto wetu hupaswa kuwa na  
nidhamu nzuri ili kumudu ushindani  
wa ajira,

**Usaili**



...kufanya maamuzi mazuri,

Njoo...upate kinywaji

Hapana,  
sitaki!



...kuwa raia wema

Asante!



...kuheshimu na kuwasaidia wengine.

Safi sana,  
William!


Asante, Farook!



Nidhamu ijengayo  
huangalia maisha  
yajayo...



Nidhamu inayojenga humaanisha kuwa  
kila mtu anawajibika kuwasaidia  
wanafunzi kujifunza na kuelewa.



Nidhamu inayojenga huwasaidia  
wanafunzi kukuza uwezo wao!



Inalenga katika kufanikisha malengo ya muda mrefu...


na si malengo ya muda mfupi..

kama vile kuwahi ili kuepuka adhabu!

Kama vile kujifunza umuhimu wa kujali muda,



Unapohamasisha nidhamu sahihi...



unapata manufaa mengi!

Mazingira mazuri ya kujifunzia!



Inamridhisha mwalimu



## Matokeo mazuri ya kujifunza...




## Sifa nzuri kwa shule!



## Manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla!



# Shule nzuri huhamasisha nidhamu inayojenga!





Je, utafanya nini ili kuhakikisha uwepo wa nidhamu ifaayo?

- Kuandaa sheria na taratibu za darasani pamoja!
- Kuchagua kamati ya nidhamu ya wanafunzi!
- Kupongeza juhudzi za wanafunzi!
- Kuacha kuchapa viboko!
- Kutumia mbinu mbadala za nidhamu!
- Kusikiliza wanafunzi!
- Kufanya utafiti kuhusu sababu za utovu wa nidhamu!
- Kuwa mfano kwa wengine!
- Kuwa na siku maalumu ya kushehereka!

### Namna ya kutumia kijitabu hiki:

- Orodhesha sifa za mtu mwenye nidhamu inayojenga
- Mwambie rafiki yako aandaе orodha kama hiyo na kisha ifananishe na ya kwako
- Soma kijitabu hiki pamoja na wanafunzi wengine au walimu na kisha jadili faida za nidhamu isiyo ya uoga
- Jadili changamoto na orodhesha mapendekezo ya utatuзи wake
- Andaa igizo kuhusu nidhamu isiyo ya uoga
- Shirikiana na walimu na wanafunzi wengine kuandaa mwongozo wa nidhamu isiyo ya uoga kwa shule nzima.

# Toa maoni, shiriki na jishindie kompyuta!

Msomaji, Serikali yako inataku kukusikia! Shiriki kwa kutuma maoni yako. Mawazo yako yanaweza kuboresha huduma kwa jamii na utawala bora. Pia, hii itakuza ushirikiano kati ya wananchi na Serikali. Maoni yako yatahusiana na **mafunzo** uliyopata kupitia kitabu hiki. Kigezo cha kupata washindi ni ubunifu au wazo jipya.



## Zawadi:



Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2012, maoni ya wanafunzi yatakayotumwa kupitia shule zao yatashindanishwa. Maoni kumi bora yatachaguliwa na yatachapishwa kwenye vitabu pamoja na tovuti. Kila shule itakayoshinda itapata kompyuta ndogo mbili (laptops).

Mwisho wa maoni yako weka taarifa zako:



- a) Tarehe
- b) Majina kamili, umri wako na jina la shule/taasisi
- c) Jinsia - Mwanaume/Mwanamke
- d) Anuani (SLP) kamili, makazi (Kata, Wilaya, na Mkoa)
- e) Simu yako na/au Barua pepe (kama unayo).



Unangoja nini! Shiriki basi kwa njia zifuatazo.  
Tuma kwa:



- Barua: OGP Ikulu, S.L.P 9120 Dar es Salaam
- Barua pepe: [ogp@ikulu.go.tz](mailto:ogp@ikulu.go.tz) au [opengovtz@gmail.com](mailto:opengovtz@gmail.com)
- Tovuti: [www.wananchi.go.tz](http://www.wananchi.go.tz)

**Fikiria. Paza Sauti. Twaweza!**



Tunawapa  
mwanga  
wandfunzi...

Kitabu hiki kimeandalisha na:



Hatuwa-  
nyanyasi!

Jadili na wenzio ulichojifunza humu  
au shiriki mjadala kuitia:



Twaweza\_Nisisi



Twaweza Tanzania

[www.twaweza.org](http://www.twaweza.org)

[www.raisingvoices.org](http://www.raisingvoices.org)